Toleo 60 - Jumad-ul-Awal 1443 AH / Januari 2022 M

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Chini ya Mfumo wa Kibepari Mtandao wa Barabara Daima ni Wenye Kukaribisha Maafa

**HABARI NA MAONI**
Covid-19 Janga la Kupangiliwa: Fursa ya Kuwakandamiza, Kuwapora na Kuwahofisha Wanadamu

**TOLEO JIPYA**
Watoto Wanazaliwa Kufa kwa Njaa nchini Afghanistan bila ya Khilafah!

**JIBU LA SWALI**
Hayakupatikana kwa Maqureshi Masharti ya Kutafuta Nusra kabla ya Ufunguzi (Fathi)



uqab.or.ke uqab_htk UQABMagazine

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 05/1443 Jumatatu, 02 Jumada I 1443 H 06/12/2021 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Chini ya Mfumo wa Kibepari Mtandao wa Barabara Daima ni Wenye Kukaribisha Maafa

Harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir inatuma rambirambi zake kwa wanafamilia na marafiki waliopoteza wapendwa wao kwenye ajali ya mto Enzui baada ya basi kutumbukia ndani ya maji, ambapo hadi kufikia sasa watu 33 wameaga dunia. Kwa majeruhi wa mkasa huu, tunawatakia afueni ya haraka.

Katika maafa kama haya, tunaweka bayana kwamba ajali huingia kwenye mzunguko wa matendo ambayo wanadamu hawawezi kuyazuia. Hata hivyo, Uislamu unaamrisha wanadamu kuwajibika ipasavyo na kuwa makini pindi wanapotenda matendo yao sawasawa wawe ni abiria ama madereva na wengineo. Uislamu aidha, unataka masuala ya usalama wa umma kupewa kipaumbele bali serikali inapaswa kuhakikishia raia wake miundo mbinu imara ili kuweko na usalama wa barabarani kwa raia wote. Isitoshe, serikali inatakikana kuweka mikakati na hatua ya kuhakikisha kuwa magari ya abiria yana vigezo vyote vya kuweko barabarani ili yaweze kutoa huduma bora ya usafiri.

Ajali hii na zile zilizotangulia zinaonesha wazi hali mbovu ya barabara ambazo kwa hakika zipo katika mazingira ya kukaribisha majanga. Kwa sababu ya ufisadi uliosheheni, kila uchao barabara hutiwa viraka na kufanya kutopitika kwa kunyesha tu marasharasha kwani hugeuka kuwa ni mito na mitego ya vifo. Cha kuhuzunisha zaidi, baadhi ya maeneo nchini hadi sasa hayana barabara nzuri huku raia ambao tayari wanasota kwa uchochole wakilimbikiziwa zigo la ushuru. Hii ndio sura halisi ya mfumo muovu wa Kibepari na tawala zake ambazo hazitilii maanani maslahi ya umma. Cha kutamausha, kwenye kung'ang'ania kwao utawala, wanasiasa wa kibepari huzunguka na Helikopta pembe zote za nchi wakifanya kampeni ya kuwinda kura lakini kwa kipindi cha mafuriko wao hubakia tu kuangalia tu runinga raia wanapokufa maji! Hii bila shaka ni hadaa kubwa ya ubepari na watawala wake wanaodharau maisha ya raia masikini.

Sisi katika Hizb ut-Tahrir tunabainisha waziwazi kwamba hali hii mbovu itaendelea kushuhudiwa chini ya mfumo fisidifu wa kibepari unaofadhilisha zaidi maslahi ya wanasiasa zaidi kuliko yale ya raia wa kawaida. Kwa hivyo tunatoa mwito kwa jamii nzima kuunga mkono kazi ya kuleta mabadiliko ya kikweli ya kuondosha mfumo wa kibepari na kuweka mahala pake mfumo safi wa Uislamu. Kwa yakini Uislamu ndio mfumo pekee unaojali maslahi ya umma yakiwemo yale ya usalama wa abiria na hii ni kuwa ni mfumo wenye sifa ya uwajibikaji katika masuala yote yakiwemo suala la usalama barabarani ya yote yanayofungamana na ukaguzi wa magari ya abiria na kutengeneza barabara nzuri.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

Afisi ya Habari Wilayah Uturuki

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 07/1443 | Jumamosi, 14 Jumada I 1443 H | 18/12/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Mnazo Nguvu! Uislamu ndio Mwelekeo Pekee wa Kutatua Migogoro Yote

Katika kipindi cha miezi miwili iliyopita, Uturuki ilikuwa ikipitia mgogoro mkubwa wa kiuchumi. Lira ya Uturuki inazidi kushuka siku baada ya siku. Ingawa Jumatano hutangaza kuwasili kwa Alhamisi, lakini sera za kimakosa zilizotekelezwa kwa miaka mingi zinapungia mwaliko wa kuribisha migogoro. Ingawa kiwango cha ubadilishaji pia kimeongezeka, maafisa wanatazama tu yanayojiri, hata mshahara wa chini uliotangazwa na Rais Erdoğan kama habari njema kwa mwaka wa 2022 unabakia chini ya kiwango cha mfumuko wa bei unaopanda. Huku idadi iliyotangazwa na Erdogan ya kima cha chini cha mshahara ilikuwa lira za Kituruki 4253.4, ambayo ilikuwa sawa na $274 wakati huo, leo ni sawa na $258. Hali hii pekee inatosha kuonesha madhila makubwa ambayo nchi hii inakumbwa nayo. Haswa kwa kupanda kwa bei kunakotarajiwa katika mwaka mpya, mshahara wa chini hautawawezesha ndugu zetu wanaofanya kazi kukidhi hata mahitaji ya kimsingi.

Matamshi ya watu wengi na ahadi, pamoja na hofu ya kisiasa katika kukabiliana na mgogoro, yanasababisha nakisi ya bajeti kuongezeka hata zaidi. Jaribio linafanywa ili kufidia nakisi ya bajeti kwa kuwekeza mtaji wa kigeni au kukopa kwa kiwango cha juu cha riba, au kwa kuchapisha pesa bila ya fidia. Uturuki imekuwa na nakisi ya bajeti tangu 1970, na inaongezeka maradufu baada ya muda. Serikali ya AKP inazidisha nakisi ya bajeti kupitia matumizi ya kiholela. Kwa ujenzi wa barabara kuu, madaraja, mikondo, mahandaki, na matumizi ya fedha kwenye viwanja vya ndege na hospitali za mijini, nakisi ya bajeti imekuwa vigumu kufidia. Bila shaka, barabara, madaraja na hospitali ambazo wananchi wanahitaji zinapaswa kujengwa, lakini ndani ya mfumo wa uwezo uliopo. Pia, uchapishaji wa pesa bila fidia na miradi inayotekelezwa kwa kutumia madeni yenye riba kubwa huileta serikali katika hatua nyingine ya maafa. Mbali na uwekezaji usio wa lazima, ufisadi, hongo, na zabuni zinazotolewa kwa bei ya kiholela na ya duni, yote yanafanya mgogoro wa kiuchumi kuwa tokeo lisiloepukika. Kwa hiyo, ufisadi na ubadhirifu ndio visababishi, na nakisi ya bajeti na mgogoro wa uchumi ndio matokeo.

Katika siku hizi ambazo mfumko wa bei unazidi asilimia 70 kulingana na takwimu zisizo rasmi, lira ya Uturuki inapoteza thamani yake siku baada ya siku, watu wanakuwa na wasiwasi kwa sababu ya gharama kubwa ya maisha, Hizb ut Tahrir inatoa suluhisho sahihi na imara kwa msingi wa kuhisi uwajibikaji. Tofauti na vyama vyengine vya kisiasa, linatokana na fikra ya Kiislamu na sio Urasilimali, ambao ndio chanzo kikuu cha tatizo.

Kwa njia hii, sisi katika Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Uturuki, tutaeleza kwa kina jinsi ya kupunguza mfumko wa bei, jinsi ya kuzuia kupanda kusiko kwa kawaida kwa viwango vya kubadilisha fedha, jinsi ya kufufua biashara pasi na wawekezaji wa kigeni, jinsi ya kuondoa vikwazo katika kilimo ambacho kinakaribia kutoweka, jinsi ya kuondoa ukosefu wa ajira, na jinsi riba na soko la hisa zinavyonyonya wafanyakazi wetu, jinsi ya kuanzisha uchumi usio na kodi, na yale ambayo rasilimali msingi za uchumi zitajumuisha . Hivi karibuni tuwagawia umma kazi yetu yenye kichwa, "Masuluhisho ya Kiislamu kwa Migogoro ya Kiuchumi katika Vifungu 10".

Katika utafiti huu tulioutayarisha kwa msingi wa mfumo wa uchumi wa Kiislamu, tunapotoa ufumbuzi wa migogoro ya kiuchumi na kimaadili, hatukwenda katika mfumo mwingine isipokuwa Uislamu. Kwa sababu Uislamu ndio mfumo pekee wenye uwezo wa kutoa masuluhisho ya kweli ya matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kimaadili. Uislamu sio Dini inayowafungia watu misikitini tu! Uislamu sio Dini iliyofungwa kati ya mtu na Mola wake! Uislamu sio Dini ambayo lazima ikumbukwe kwenye hafla za kidini! Bali Uislamu ni mfumo unaoelekeza nyanja zote za maisha. Uliwanyanyua Waislamu zamani na kuwanyanyua kutawala dunia. Uislamu leo bado una nguvu ile ile! Kwani mfumo wa uchumi wa Kiislamu ndio njia pekee ya wokovu si kwa Waislamu tu bali pia kwa wanadamu wote walionaswa katika makucha ya urasilimali, ambao uliwafanya kupoteza hisia zao za huruma. Nyinyi si wanyonge! Kwa sababu Uislamu ndio mwelekeo pekee wa kutatua migogoro yote.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Uturuki**



Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI

# Covid-19 Janga la Kupangiliwa: Fursa ya Kuwakandamiza, Kuwapora na Kuwahofisha Wanadamu

**Habari:**

Serikali duniani kote zinashughulika hivi sasa kuweka mikakati ya kikatili ili kudhibiti kuenea kwa aina mpya ya Virusi vya Ugonjwa wa Korona vya 2019 kwa jina Omicron.

**Maoni:**

Tangu kutokea kwa mkurupuko wa janga la kupangiliwa mnamo mwanzoni mwa 2019 hadi sasa mwenendo wa maisha ya wanadamu yamebakia kupinduliwa juu chini. Maamuzi yasioingia akilini yenye ushawishi wa makampuni machache yanaendelea kusababisha matatizo ulimwenguni kote. Makampuni hayo yameasisiwa juu ya msingi mmoja muhimu nao ni kupatiliza matatizo ya watu ili kujilimbikizia faida kupitia kutunga na kutekeleza sheria na sera zenye mashaka kwa jina kupambana na janga la kupangiliwa la Covid-19.

Makampuni hayo yamekazanisha vitanzi vyao juu ya miundo mbinu ya afya ulimwenuni kote kiasi kwamba hakuna kiongozi wa serikali anayeweza kuwauliza swali pasina na kutarajia kushambuliwa kwa madhara. Hivyo basi, asasi za serikali ulimwenguni zinayasifu makampuni hayo katika juhudi zao za kutengeneza na kusafirisha chanjo. Haishangazi kwamba wale wanaodhaniwa kuwa ni vikwazo hung'olewa kwa haraka kutoka madarakani kwa kutumia njia yoyote ile, kwani lengo huhalalisha njia!

Serikali ambazo zilidai kuwa zinafurahia ubwana na uhuru usiokuwa na mipaka zimejipata kuwa zinatumika kama vikaragosi na makampuni hayo. Kwa kuwakandamiza raia zao kupitia kuwafungia, kuwapora kupitia kutumia rasilimali za umma katika kununua chanjo ambazo uwezo wake unatiliwa shaka na athari zake mbaya zikowazi kabisa. Kwa kuongezea wale ambao wamekataa kuchukua chanjo hizo wanadunishwa na kuhofishwa kwa kunyimwa huduma na wengine kutishiwa kuwa watafutwa kazi miongoni mwa dhulma nyinginezo.

Janga la kupangiliwa la Covid-19 ni ajenda ambayo lengo lake msingi ni kuleta mabadiliko hadaifu kupitia kupangilia upya nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo matokeo yake yanajulikana pekee na makampuni yaliyochochea. Wenye nguvu na wasiokuwa na nguvu wote wamemezwa na njama ovu na za kilafi za kipote cha watu wachache wanaodai kuwa wanawajali wanadamu. Alas! Wanachojali zaidi ni kuwaangamiza wanadamu kwa kutia faida kupitia shida zao.


Wakati ni sasa kwa kila mtu mwenye akili timamu kuungana na kusema LA kwa hizi sheria na sera nyingi zisizoingia akilini za kikatili ambazo zinayakaba maisha yetu. Kwa kusimama pamoja ni hatua katika mwelekeo sahihi kwa kuziambia serikali zetu kwamba imetosha kufanya biashara na makampuni yaliyo na njaa ya faida. Kwa kuongezea, tutakuwa tunayaambia makampuni yanayo furahia ulinzi wa kisheria kutokamana na bidhaa wanazozitengeza kwamba SISI SIO WANYAMA WA KUTUMIKA KATIKA MAJARIBIO!

Kimsingi, lazima tujifunge na ulinganizi wa kurudisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Kutokuwepo kwa Khilafah kumetoa mwanya kwa makampuni haya kuwepo na kuhangaisha wanadamu. Kwa kuongezea, kuwepo kwao kunaungwa mkono na viongozi wa kirasilimali wa kisekula ambao wameziuza roho zao kwa shetani kwa malipo ya vijipesa wanavyopewa na makampuni hayo.

Khilafah ni ngao na mlinzi ambaye kuwepo kwake ni kwa ajili ya kutekeleza Shari'ah ya Kiislamu ambayo vyanzo vyake ni Qur'an, Sunnah, Makubaliano ya Maswahaba na Qiyas. Hivyo basi, msingi wa ujenzi wake na kipimo cha vitendo vya wanadamu utakuwa ni Halal na Haram, na sio faida au hasara. Kwa msingi huo Khilafah haitokubali kuwepo kwa majanga ya kupangiliwa katika himaya yake. Hata hivyo, kunapotokea janga itakwenda mbio kukabiliana nalo na sio kunufaika kupitia kwake kwa kushirikiana na baadhi ya washikadau katika sekta ya afya kama inavyohushudiwa hivi sasa. Kwani utafiti huru unaendelea kuthibitisha kwamba Covid-19 ni janga la kupangiliwa na SIO janga kama inavyodaiwa na wanaotia faida ambao wanatumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kueneza uongo wao ili kupata mauzo zaidi!

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**





Email: info@uqab.or.ke

# Watoto Wanazaliwa Kufa kwa Njaa nchini Afghanistan bila ya Khilafah!

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammed**



BBC iliripoti mnamo tarehe 2 Disemba kwamba miundombinu inayoporomoka ya Afghanistan imesababisha kukaribia kutoweka kwa mfumo wa huduma za afya na ustawi wa jamii.

Madaktari wengi sasa wanafanya kazi bila malipo na janga la chakula limeongeza mzigo usio na kifani kwa hospitali zinazofurika wananchi wanaoteseka kutokana na hali mbaya ya umaskini.

Dkt Nuri daktari wa uzazi anayefanya kazi eneo la Afghanistan ya Kati aliripoti kisa cha mama mmoja ambaye aliomba mauti kabla tu ya kujifungua kwa upasuaji. Alikuwa akililia msaada bila kuelewa jinsi angeweza kumtunza mwanadamu mwingine wakati yeye mwenyewe alikuwa na utapiamlo sana hivi kwamba hangeweza kutoa maziwa ya kutosha kwa mtoto mchanga. Nukuu yake ni kama ifuatavyo; "Wodi ya wajawazito ni mojawapo ya wodi zenye furaha zaidi katika hospitali yoyote, lakini sivyo tena nchini Afghanistan, mnamo Septemba nilitazama watoto watano waliozaliwa wakifa kwa njaa. Ni kama kuzimu humu ndani."

Mgogoro huu mbaya ambapo Umoja wa Mataifa unanukuu watoto milioni 14 wako katika hatari ya njaa. Jumuiya ya Kimataifa imezuia ufadhili na misaada ya nje ili kuadhibu uongozi wa Taliban na hivyo kutumia fedha kama silaha ya vita dhidi ya Waislamu.

Dkt Siddiqi anayefanya kazi jijini Kabul alishuhudia watoto 4 walio chini ya miaka 10 wakifa kila wiki katika hospitali yake sio tu kutokana na maradhi yanayohusiana na udhaifu bali kwa kula sumu inayotokana na chakula duni.

Hili ni janga ambalo linatolewa kimkakati na mataifa ya kikoloni yanayosimamia uzuiaji wa utawala wa Kiislamu duniani. Kuwaweka watu kwenye ukingo wa mauti ni ala ya kuwazuia kufanya kazi kwa ajili ya mwamko wa Kiislamu. Lakini Mwenyezi Mungu (swt) ameahidi kwamba daima kutakuwa na kheri katika Ummah Wake (swt). Kamwe hatuwezi kuweka chochote juu ya uwezo wa Mola wa walimwengu wote;

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللّهِ

**"Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu..."** [Aali-Imran 3:110].

Umaskini ulioratibiwa ni maagizo ya sawia yanayoweza kuonekana nchini Yemen, Syria na maeneo mengine muhimu ambapo udhibiti wa kisiasa ni muhimu mno kwa utawala wa Magharibi.

Wanachohitaji watoto wasio na hatia wa ulimwengu ni kiongozi wa kweli wa kuwakomboa kutokana na umaskini na ukosefu wa mgao wa rasilimali wa kulazimishwa. Amiri wa Khilafah angehakikisha mara moja kwamba mahitaji ya kimsingi yanatolewa kwa haki kwa wote bila ya hatari ya makusudi kwa mtoto au masikini hata mmoja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwamba Umma wa Muhammad (saw) ufanye kazi ili kuleta jambo hili kuwa ni jambo la dharura kubwa zaidi.



Email: info@uqab.or.ke

**JIBU LA SWALI**

# Hayakupatikana kwa Maqureshi Masharti ya Kutafuta Nusra kabla ya Ufunguzi (Fathi)



**Swali:**
Assalamu alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuhu,

Sheikh wetu, nina swali lau utaniruhusu, yajulikana kuwa Mtume (saw) alitafuta Nusra kwa makabila, lakini je, Maqureish walikuwa miongoni mwa makabila ambayo Mtume (saw) alitafuta Nusra kwao?

Na Mwenyezi Mungu awalipe kheri.

**Jibu:**
Waalaykum salam Warahmatullahi Wabarakaatuhu

Utafutaji wa Nusra huwa kwa yule ambaye anaitikia mwito wa Uislamu na kuslimu... Akawa katika watu wa nguvu na hifadhi kwa namna ambayo itamuwezesha kuunusuru Uislamu na kusimamisha Hukmu kwa alichokiteremsha Mwenyezi Mungu. Haya masharti mawili ni wajibu yapatikane kwa yule inayotafutwa Nusra kwake. Ikiwa hakuitikia mwito wa Uislamu akaslimu, au hakuwa miongoni mwa watu wa nguvu na himaya inayoweza kuathiri mageuzi, yeye peke yake na kabila lake au pamoja na wengine, basi hawezi kuwa katika watu wa Nusra... na Maqureysh hayakupatikana kwao hayo kabla ya ufunguzi (Fathi), kwani watu wa nguvu na himaya hawakusilimu katika mji wa Makkah ambao walikuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko, hivyo Mtume (saw) hakutafuta Nusra kwao, bali alikuwa akilingania Uislamu ndani ya Makkah na wale waliosilimu walikuwa ni madhaifu, na baadhi ya wenye nguvu lakini kibinafsi pasi na makabila yao, hivyo hawakuweza kuleta mabadiliko kama Umar na Hamzah.

Kwa hiyo hakukuwa na utafutwaji wa Nusra kutoka kwa watu wa Makkah kwa kutopatikana masharti hayo mawili, bali mjini Makkah kulikuwa na Daawah kwa Uislamu, Na hakukuwa na mwitiko kwa Uislamu kutoka kwa watu wa nguvu na himaya ndani ya Makkah wenye uwezo wa kuleta mabadiliko; hivyo basi hakukuwa na Talab An-Nusrah (ufafutwaji wa Nusra) mjini Makkah, bali Makkah ilikombolewa kwa ufunguzi.

Kwa hivyo Mtume (saw) alikuwa akijitambulisha kwa makabila yenye nguvu na himaya na kuwalingania kwa Uislamu kwanza kisha kutafuta Nusra kwao wanaposilimu. Haya hapa ni baadhi ya yaliokuja juu ya hayo katika Seera:

**Kwanza:** kutoka katika Sira ya Ibnu Hisham:

1- Utafutaji wa Nusra kutoka kwa Thaqif:

[Amesema Ibn Ishaq: Alipokufa Abu Twalib Maqureysh walimfanyia maudhi Mtume (saw) ambayo hawakuwahi

Endelea... UK 7


Email: info@uqab.or.ke

kumfanyia katika uhai wa ami yake Abu Twalib, Akatoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kwenda Twaif, akitafuta Nusra kutoka kwa Thaqif, na himaya kwao dhidi ya watu wake, Na akitarajia wamkubalie alichokuja nacho kutoka kwa Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla,Akatoka kuwaendea akiwa pake yake.

Asema Ibn Ishaq: Yazid bin Ziyad alinihadithia, kutoka kwa Muhammad bin Kaa'bi Al Quradhiy, Asema: Mtume (saw) alipofika Twaif, alikusudia kundi la Thaqif, Hao walikuwa wakati huo ni mabwana wa Thaqif na masharifu wao, nao ni ndugu watatu: Abd Yaleel bin Amr bin Aasw, Masu'd bin Amr bin Umair, na Habib bin Amr bin Umair bin Awf bin U'qdata bin Ghayrata bin Awf bin Thaqif. Na mmoja wao alikuwa na mwanamke wa Kiquresh kutoka Banu Jumah, Mtume (saw) akaketi nao na kuwalingania kwa Mwenyezi Mungu, akazungumza nao juu ya yale aliyowajia ya kumnusuru kupitia Uislamu, na kusimama naye dhidi ya watakaomkhalifu katika watu wake. Mmoja wao akamwambia: angeirarua nguo ya Kaa'ba ikiwa Mwenyezi Mungu ametumiliza, akasema mwengine: "Kwani Mwenyezi Mungu hukupata mwengine wakumtumiliza asokuwa wewe?", Akasema watatu: "Wallahi kamwe sitozungumza na wewe!, kwani ikiwa wewe ni Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama unavyosema, basi wewe ni hatari kukurudishia maneno, na ikiwa wamsingizia Mwenyezi Mungu uongo, basi haifai mimi kuzungumza na wewe", Mtume (saw) akasimama kutoka kwao akiwa amekata tamaa na kheri ya Thaqif.

2- Mtume kujitambulisha kwa Banu Aamir Ibn Swa'swa'ah

Asema Ibn Ishaaq: Al zuhriy amenihadhia kwamba Mtume (saw) aliwaendea Banu Aamir bin Swa'swa'h, akawalingania kwa Mwenyezi Mungu Azza wa Jalla, akijtambulisha kwao. Akasema mtu miongoni mwao- anayeitwa: Bayharata bin Firaas, asema Ibn Hishaam: Firaas bin Abdillah bin Salamata (Al khayr) bin Qushair bin Kaa'bi bin Rabii'ata bin Aamir bin Swa'swa'h: "Wallahi lau mie ningemchukua huyu kijana wa Kiquresh, ningewatafuna Waarabu kupitia kwake", kisha akasema: "Je, waonaje sisi tukikupa Kiapo cha utiifu (Baya'h) juu ya jambo lako kisha Mwenyezi Mungu akakupa ushindi dhidi ya wanaokukhalifu, je, jambo hili litakuwa kwetu baada yako?" Akasema (saw):

الْأَمْرُ إِلَى اللهِ يَضَعُهُ حَيْثُ يَشَاءُ

**“Jambo hili lipo kwa Mwenyezi Mungu analiweka atakapo.”** Akasema: akamwambia: Je, walenga shingo zetu tuzitoe muhanga kukulinda wewe dhidi ya Waarabu, kisha Mwenyezi Mungu akikupa ushindi jambo liwe kwa wasiokuwa sisi? Basi hatuna haja na jambo lako, wakamkatalia...]

**Pili:** kutoka kwa kitabu cha Al-Bidaya Wa Al-Nihaya cha Ibn Kathir Al Dimishqiy

[Asema: "Kisha tukafika katika mkao wenye utulivu na heshima, mara tukawaona wazee wenye vyeo na mapambo, akatangulia Abubakar akasalimia - Asema Ali: na Abubakar alikuwa akitangulia katika kila kheri - Abubakar akawaambia: Ni kaumu gani nyie? Wakasema: Ni kutoka Shayban bin Thaa'laba, akamgeukia Mtume (saw) akasema: "Bi Abi anta wa ummi" (Neno linaloashiria heshima na kujitolea muhanga kwa ajili ya Mtume (saw) baada ya hawa hakuna izza katika jamii yao.

Na katika riwaya: Watu wao hawana udhuru baada ya hawa, Hawa ndio nyota ya asubuhi katika watu wao, hawa ni nyota ya asubuhi.

Na katika miongoni mwa alikuwemo Mafruq bin Amr, Hani bin Quswaybah, Muthanna bin Haarithah, na Nuu'man bin Sharik, na aliyekuwa karibu na Abubakar katika Jamaa ni Mafruq bin Amr, Na Mafruq bin Amr aliwashinda katika uzungumzaji na ufasaha, na alikuwa na tezi mbili zinazoanguka kifuani mwake, na alikuwa amekaa karibu zaidi na Abubakar katika Jamaa wote.

Abubakar akamwambia: "Vipi idadi yenu?" Akasema: "Sisi twazidi Alfu na Alfu hawashindwi kwa uchache". Akamwambia: "Je, vipi nguvu zenu na himaya?" Akasema: "Ni juu yenu juhudi na kila watu wana bidii". Akasema Abubakar: "Je vita ni namna gani kati yenu na maadui zenu?" Akasema Mafruq: "Hakika sisi ni wakali katika mapambano tunapokasirika, sisi twatanguliza farasi wa kivita kuliko watoto, na silaha kuliko mashamba, na Nusra ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu mara anatupa ushindi mara tunashindwa inaonekana kana kwamba wewe ni ndugu wa Kiqureshi?" Akasema Abubakar: "Ikiwa mumefikiwa na habari kuwa Maqureish wana Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu basi huyu hapa". Akasema Mafruq: "Hakika tumefikiwa na habari kuwa yanatajwa hayo je walingania nini ewe ndugu Mqureshi?", kisha akamgeukia Mtume (saw), akaketi Abubakar akasimama akamfunika kwa nguo yake. Mtume (saw) akasema:

أَدْعُوكُمْ إِلَى شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَنِّي رَسُولُ اللَّهِ، وَأَنْ تؤوونى وَتَنْصُرُونِي حَتَّى أُؤَدِّيَ عَنِ اللهِ الَّذِي أَمَرَنِي بِهِ، فَإِنَّ قُرَيْشًا قَدْ تَظَاهَرَتْ عَلَى أَمْرِ اللَّهِ، وَكَذَّبَتْ رَسُولَهُ، وَاسْتَغْنَتْ بِالْبَاطِلِ عَنِ الْحَقِّ، وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

**"Nawalingania kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee hana mshirika, na kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na mnipokee na kuninusuru mpaka niweze kutekeleza yale ambayo Mwenyezi Mungu ameniamrisha kwayo, kwani Maquresh wamepinga Amri ya Mwenyezi Mungu, na wakamkadhibisha Mtume wake, na wakatosheka na batili badala ya haki, na Mwenyezi Mungu ametosheka na ni Mwenye kusifiwa".**

Akasema: Na huyu ni Muthanna Mzee wetu na bwana

*Endelea... UK 8*

wa vita wetu. Akasema Al Muthanna: "Nimesikia maneno yako na nikaona uzuri wa kauli yako ewe ndugu wa Kiquresh, na yamenifurahisha uliyoyaongea. Na Jibu langu ni Jibu la Hani bin Qubaysah; tukiwacha dini yetu na kukufuata kwa mkao uliokaa nasi basi itakuwa tumeshukia kati ya mistari miwili mmoja ni Yamama, na mwengine ni Al samawa. Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

وما هذان الصريان؟

**“Mistari hii miwili ni ipi?”**

Akamwambia: Ama mmoja wapo: ardhi yenye nguvu na ardhi ya Waarabu, ama nyengine: Ni ardhi ya Fursi na mito ya Kisraa, tumeingia katika ahadi ambayo aliichukua kwetu Kisra kuwa tusifanye chochote, wala tusimhifadhi mgeni. Huenda hili jambo unalotulingania ni katika linalochukiwa na wafalme, ama kwa upande wa biladi za Kiarabu basi hatia ya mmiliki husamehewa na udhru wake haukubaliki.

Ukitaka tukunusuru na kukulinda upande wa Waarabu basi tutafanya. Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

ما أسأتم الرد إذ أفصحتم بالصدق، إنه لا يقوم بدين الله إلا من حاطه من جميع جوانبه

**“Majibu yenu sio mabaya kwa kusema kwenu ukweli, Hakika hasimami na Dini ya Mwenyezi Mungu ila yule ambaye ataizunguka kwa pande zote.”]**

4- Kisha ikawa Bay'ah ya Aqabah ya kwanza na ya pili na kufuatiwa na Hijra na kusimamisha kwa Dola. Na tamati ni kuwa Hakika kuwa tayari na kumnusuru Mtume wa Mwenyezi Mungu hakukupatikana katika watu wenye nguvu na hifadhi mjini Makkah ndani ya Miaka ya mwanzo ya Mtume (saw). Hakukupatikana kwao Uislamu kisha maandalizi ya kumnusuru Mtume (saw) kwa hiyo Mtume (saw) hakutaka Nusra yao ili kusimamisha Dola katika Makkah kupitia njia ya Nusra, akaitafuta kwa wale ambao yapatikana kwao fursa ya kuitikia Uislamu na wawe katika (Ahlil quwwah wal mana'h) watu wenye nguvu na mamlaka wanaoweza kuleta mabadiliko. Wakapata Maanswar Utukufu huu mkubwa Duniani na Akhera na huko ndiko kufuzu kukubwa. Kisha baada ya hapo Dola ya Kiislamu ikaikomboa Makkah kwa ufunguzi.

Nataraji haya yanatosheleza na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi na Mwenye hekima.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Rashtah**

**06 Safar 1443 H**

**13/09/2021 M**